# MAJI TANZANIA

1 - 5 - 7 - 5 Tupo Site Kikazi Zaidi

Toleo 032

Aprili - Julai 2026


Haliuzwi

## Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Balozi Dkt Emmanuel Nchimbi** ameitaka Wizara ya Maji kutekeleza Miradi ya Maji kwa kulinda ardhi oevu nchini.



### Mhe. Balozi Dkt Emmanuel Nchimbi

Makamu wa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Akibonyeza Kitufe kama ishara ya kuzindua program endelevu ya Usimamizi wa Mazingira kuelekea Dira ya mwaka (2050), katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.





ziwa Victoria ni rasilimali ya pamoja inayopaswa kulindwa na kuhifadhiwa kwa ushirikiano wa kikanda kutokana na mchango wake mkubwa katika uchumi, biashara, mazingira, usalama na maisha ya wananchi.



# Wizara ya Maji Yatakiwa Kutekeleza kwa Kuzingatia Uhifadhi wa Ardhi Oevu

**Dodoma,** Tanzania

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt Emmanuel Nchimbi ameitaka Wizara ya Maji kutekeleza miradi ya maji kwa kulinda ardhi oevu nchini.

Ametoa agizo hilo katika Siku ya Mazingira iliyofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.

Mhe. Dkt. Nchimbi amemwakilisha Rais katika maadhimisho hayo.

Amesema hadi kufika mwaka 2050 Tanzania inakadiriwa kuwa na idadi ya watu zaidi ya milioni 100 hivyo, utunzwaji wa ardhi oevu utasaidia kuendeleza vyanzo vya maji na kupunguza upungufu wa maji.

Pia, ametoa agizo pia kwa Wakala wa Misitu Nchini (TFS) kuhakikisha miti ya kutosha inaoteshwa katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kutunza mazingira na vyanzo vya maji.

Dira ya mwaka 2050 imejumuisha maendeleo ya mazingira na uhifadhi wa ardhi oevu Nchini.

Katika maagizo mengine makamu wa Rais ameziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuanzisha bustani za kijani na kuzitunza kikamilifu.

Maadhimishi ya Siku ya Mazingira yamehusisha uzinduaji wa program endelevu ya Usimamizi wa Mazingira kuelekea Dira ya mwaka (2050) ambayo itatekelezwa kuanzia mwaka 2026 mpaka mwaka 2030.





# SERIKALI YATAKA ULINZI NA UHIFADHI WA ZIWA VICTORIA

**Serikali imesisitiza umuhimu wa ulinzi wa ziwa Victoria kwa maendeleo ya wananchi.**

**Mwanza**, Tanzania

Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb) amesema hayo katika maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Ziwa Victoria yaliyofanyika katika viwanja vya Nanenane Nyamhongolo jijini Mwanza,.

Dkt. Nchemba, mgeni rasmi wa siku hiyo, amesema ziwa Victoria ni rasilimali ya pamoja inayopaswa kulindwa na kuhifadhiwa kwa ushirikiano wa kikanda kutokana na mchango wake mkubwa katika uchumi,

"

*Ziwa Victoria si mali ya nchi moja. Ni rasilimali inayotuunganisha kama jumuiya na tunapaswa kushirikiana katika kulinda mazingira, usalama na uchumi unaotegemea ziwa hili,"* **Dkt. Nchemba** amesema.

Amesema maadhimisho hayo yanapaswa kuwa sehemu ya kuhamasisha usimamizi



endelevu wa rasilimali za maji, kuimarisha mshikamano wa kikanda pamoja na kuongeza uwajibikaji wa pamoja katika kulinda mazingira ya ziwa Victoria kwa manufaa ya kizazi

Amesisitiza umuhimu wa kuimarishwa kwa mifumo ya usalama na uokoaji majini pamoja na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika kufuatilia shughuli za uvuvi, ubora wa maji na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ametoa wito kwa taasisi za utafiti kuendelea kufanya tafiti zitakazosaidia kupata suluhisho la changamoto zinazoathiri mazingira ya ziwa Victoria ikiwemo ongezeko la magugu maji na uharibifu wa vyanzo

Aidha, Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya Maji katika Kanda ya ziwa pamoja na kuimarisha juhudi za kulinda na kuhifadhi ziwa Victoria ambalo ni nguzo muhimu ya uchumi, usalama na maendeleo ya wananchi.



Sanjari na hayo Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri amesema Tanzania imekuwa mwenyeji wa kwanza wa maadhimisho hayo kufuatia maamuzi ya Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Amesema maadhimisho hayo yamehusisha shughuli mbalimbali ikiwemo kuotesha miti, maonesho ya wadau wa Sekta ya Maji pamoja na mijadala kuhusu uhifadhi wa Ziwa Victoria.

Kaulimbiu ya maadhimisho ni : “Maji Yetu, Mustakabali Wetu: Tuungane kwa Uendelevu wa Bonde la Ziwa Victoria" na yamehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, wananchi, wadau wa Sekta ya Maji pamoja na wageni kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.





# SERIKALI KUMALIZA KERO YA MAJI KIBAIGWA - KONGWA

**Kongwa,** Dodoma

Serikali imewahakikishia wakazi wa Kata ya Kibaigwa, Wilayani Kongwa, kumalizika kwa changamoto ya upatikanaji wa majisafi, kufuatia mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita wa kununua mitambo ya kisasa ya kuchimbia visima na ujenzi wa mabwawa kwa kila mkoa nchini.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), amesema wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara kwenye stendi ya mabasi ya Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa.

Akifafanua jitihada za Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya maji, Dkt. Nchemba alibainisha kuwa hatua ya awali ya upatikanaji wa mitambo imekamilika, na sasa Serikali inaelekeza nguvu kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa.

"Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshakamilisha ununuzi wa mitambo ya kuchimbia visima kwa kila mkoa. Hatua inayofuata sasa ni kutenga Bajeti mahususi ya kununua vifaa na kuanza kutekeleza miradi mikubwa ya maji itakayomaliza kero hii kwa wananchi wa Kibaigwa na maeneo ya jirani," alisema Dkt. Nchemba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph, ameshiriki kikamilifu katika kuhakikisha maelekezo ya Serikali yanatekelezwa kwa manufaa ya Wananchi wa Kibaigwa.

Waziri Mkuu yupo katika ziara ya kikazi ya siku mbili katika Wilaya za Kongwa (Kibaigwa) na Mpwapwa. Lengo kuu la ziara hiyo ni kukagua miradi ya maendeleo, kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.






# BWAWA LA FARKWA MRADI WA KIMKAKATI WA HUDUMA YA MAJI, MKATABA WASAINIWA

**Farkwa,** Dododma

Waziri Wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema ujenzi wa bwawa la Farkwa ni mpango kabambe wa Serikali kuhakikisha changamoto ya maji katika jiji la Dodoma na maeneoJirani

Ametoa kauli hiyo katika hafla ya kusaini ujenzi wa bwawa la Farkwa katika kijiji cha Bubutole kata ya Farkwa Wilaya Chemba mkoani Dodoma.

Ameeleza gharama ni shilingi bilioni 163.43 mpaka kukamilika kwake, na litaondosha changamoto ya maji Jijini Dodoma, likiwa na uwezo wa kuhifadhi lita za ujazo zaidi ya billion 400.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amesema kuwa mradi huo utahusisha ujenzi wa bwawa kuu lenye mita 1300, kimo cha mita 32, pamoja na bwawa dogo lenye urefu wa mita 1600 na kimo cha mita 15 Ili kuzuia upotevu wa Maji.

Bwawa hilo likikamilika litakuwa na uwezo wa kutoa maji mita za ujazo 7236 kwa siku.

Aidha kutakuwa na mtambo wa kutibu maji wenye uwezo wa kuzalisha maji kwa siku mita za ujazo 128,000.

Ameongeza, sio tu kupata maji pekee bali pia kufungua fursa za ufugaji wa samaki kuongeza usalama wa chakula na kipato kwa wananchi.

Mradi huo unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mkandarasi akiwa kampuni ya China Jiang Chi International ya China na muda ukiwa kipindi cha miezi 22, kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Wananchi wanaoathiriwa na mradi wanapata makazi bora,





# WAZIRI AWESO ATOA AGIZO MAHSUSI KUDHIBITI MAJI YASIYOLIPIWA

**Dodoma,** Tanzania

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb.) amezitaka Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini kuhakikisha zinafanya kazi ya kuthibiti maji yasiyolipiwa (NRW) katika maeneo wanayotoa huduma.

Amesema tathmini iliyofanywa na Wizara ya Maji imebaini yapo baadhi ya maeneo yapo vizuri na baadhi ya maeneo yana changamoto ya upotevu wa maji.

Ameyasema hayo wakati akizindua bodi ya 10 ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) na kusisitiza moja ya kipimo cha utendaji kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji ni suala la kusimamia udhibiti wa upotevu wa maji.

“Niwaombe na niwasihi sana watendaji wa Mamlaka zetu za maji twendeni tukadhibiti upotevu wa maji, faraja ya Mkurugenzi wa maji ni wananchi kupata maji,” Mhe. Aweso amesema.



Ameongeza kuwa jambo ambalo halimfurahishi ni upotevu wa maji, akisisitiza kuwa faraja yake kubwa ni huduma hiyo kuwafikia wananchi na sio kupotea.

Waziri Aweso ameomba ushirikishwaji wa viongozi wa mikoa na wilaya kupitia kamati za ulinzi na usalama katika wa miundombinu ya maji wanashitakiwa kwa taratibu zilizopo.



# AGENDA YA MAJI 1,575 YATUA UN

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amewasilisha agenda ya maji ya 1,575 katika mazungumzo na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Mhe. Li Junhua anayeshughulikia masuala ya Uchumi na Jamii.

Kikao hicho kimefanyika pembezoni mwa Mkutano wa Nne wa Umoja wa Mataifa kuhusu Maji na Maendeleo uliofanyika katika jiji la Dushanbe nchini Tajikistan.

Waziri Aweso ameeleza mkakati wa Serikali wa kupeleka huduma ya majisafi katika vijiji vilivyobaki 1,575. Vijiji hivyo vinahitaji miundimbinu rasmi ya huduma ya maji kwa wananchi, pia ametumia wasaa huo kutoa mwaliko kwa Umoja wa Mataifa kushirikiana na Tanzania.

Ameeleza hatua zinazochukuliwa na Tanzania kama sehemu ya Dunia inavyoguswa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi na inavojidhatiti na uhitaji wa ushirikiano kutoka Umoja wa Mataifa.

Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa Mhe. Li ameihakikishia Tanzania ushirikiano katika kutatua changamoto za maji na kuahidi kutoa ushirikiano katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na athari zake kwa rasilimali za maji.



# WADAU WA MAENDELEO WAMEALIKWA NCHINI TANZANIA KUWEKEZA KATIKA SEKTA YA MAJI.

**Dushanbe**, Tajijistan

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), ametoa mwaliko akimwakilisha Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba katika Mkutano wa Nne wa Kimataifa wa Maji na Maendeleo Endelevu jijini Dushanbe nchini Tajikistan.

Amebainisha kuwa Tanzania inakamilisha utoaji wa huduma ya majisafi katika vijiji 1575 ambavyo havijapata huduma kati ya vijiji 12,333.

Amebainisha umuhimu wa kujenga uwezo wa Kitaasisi, matumizi ya teknolojia na utafutaji wa vyanzo mmbadala vya fedha katika Sekta ya Maji.

Waziri Aweso ameihakikishia Jumuiya ya Kimataifa kuwa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 Toleo la 2025 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 zimefungua mlango kwa ushiriki wa Sekta Binafsi katika masuala ya maji nchini.



# UONGOZI WA MWAUWASA WAWEKWA KANDO

**Mwanza**, Tanzania

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), ameiweka kando Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kwa kutoridhishwa na kiwango cha utoaji huduma ya majisafi na salama kwa wateja jijini Mwanza.



Hatua hiyo imefuatia ziara ya kikazi iliyofanyika na kubaini uwepo wa changamoto za upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi, chanzo kwa kiwango kikubwa ikiwa ni udhaifu wa kiutendaji na weledi kazini.

Waziri Aweso amesema anasuka timu mpya ambayo itawajibika kikamilifu katika kuboresha huduma ya maji Jijini Mwanza.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri katika tukio hilo ameainisha kuwa Serikali inachukua hatua kwa watumishi ambao hawazingatii taratibu na kuwajibika kazini.



# WIZARA YA MAJI KUIMARISHA USTAWI WA WATUMISHI – AWESO

**Mtumba**, Dodoma

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amesema Wizara ya Maji itaendelea kushirikiana na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) ili kuimarisha ustawi na maendeleo ya watumishi wa Sekta ya Maji.

Akishiriki katika baraza la Watumishi wa Wizara ya Maji katika Kikao cha Pili , Mji wa Serikali – Mtumba, jijini Dodoma, Aweso amesisitiza kuwa watumishi ndio mhimili mkuu wa mafanikio ya sekta hiyo na kutambua mchango wao mkubwa katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Ameeleza kuwa Wizara inathamini mchango wa watumishi wake na itaendelea kuchukua hatua za kusimamia haki zao za msingi, ikiwemo ustawi na maendeleo yao. Amebainisha kuwa ushirikiano na TUGHE utaimarishwa katika ngazi zote za tawi, mkoa na taifa kwa lengo la kulinda maslahi ya watumishi wa Sekta ya Maji.

"Wizara ya Maji ina watumishi wenye uwezo mkubwa, jambo linalotusaidia kufikia malengo yetu ya kisekta. Sisi viongozi tutaendelea kusimamia haki zenu za msingi, ikiwemo ustawi na maendeleo yenu," Aweso amesema.

Aidha, Waziri Aweso amewataka watumishi kuzingatia nidhamu ya kazi kwa kujituma na kujitoa kikamilifu, badala ya kufanya kazi kwa woga. Pia, amesisitiza umuhimu wa uwajibikaji katika maeneo yote ya kazi ili kuongeza ufanisi na tija.

Vilevile, amesisitiza umuhimu wa ushirikishwaji wa watumishi wote bila kujali kada au vyeo, akibainisha kuwa kutoa nafasi kwa kila mmoja kutoa maoni ni msingi wa mafanikio ya sekta. Ameongeza kuwa Wizara itaendelea kutoa motisha na kutambua watumishi wanaofanya kazi kwa bidii, pamoja na kuboresha mazingira ya kazi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, amemshukuru Waziri Aweso na watumishi wote kwa ushirikiano wao katika kufanikisha malengo ya taasisi.

"Mafanikio tuliyoyapata katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni kielelezo cha umoja na mshikamano wetu. Huu ndio msingi mkuu wa mafanikio yetu," Mhandisi Mwajuma amesema.



Aidha, alieleza kuwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali, Menejimenti ya Wizara inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuzitatua kwa manufaa ya watumishi na taasisi kwa ujumla.





# ZAMCOM WAKUTANA TANZANIA

Maji ya kimataifa ni moja ya rasilimali inayoleta amani katika nchi mbalimbali zinazonufaika na wananchi wake.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso ( Mb) akifungua kikao cha 13 cha  Baraza la Mawaziri la Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (ZAMCOM) jijini Dar es salaam amesema maji hayana mpaka na yanakusanya watu kwa maendeleo yao.



Mhe. Aweso ambaye ni mwenyekiti wa ZAMCOM anayemaliza kipindi chake ameainisha kuwa umoja wa wananchi na nchi walizopo umeletwa na maji ya kimataifa, maji yanayovuka mipaka ya nchi zao.




Amesema ni muhimu kuwa na rasilimali za kutosha ili kuleta maendeleo na wananchi wanashirikishwa kutunza rasilimali za maji ili kuleta maendeleo katika sekta nyingine za uchumi.

Mhe. Aweso amesisitiza kwa wajumbe wa mkutano huo kuwa maji ni muhimu na yanahitajika kuleta maendeleo kwa wananchi.

ZAMCOM inagusa maisha ya kila wananchi zaidi ya milioni 51 na imekusanya nchi za Tanzania, Angola, Zambia, Malawi, Namibia, Botswana, Zimbabwe, na Msumbiji.

Kufuatia kikao cha Dar es salaam na utamaduni wa kazi wa ZAMCOM nchi ya Zambia imekabidhiwa kijiti cha Mwenyekiti pamoja na Zimbawe ikiwa makamu wake.




# WAZIRI MKUU AWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA MIJI 28 CHAMWINO

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Mwigulu Nchemba ameweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa miji 28 wenye thamani ya Shillingi bilioni 17.2, katika mji wa Chamwino, mkoani Dodoma.

Amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi za mradi huo wa maji, na kuipongeza Wizara ya Maji kwa kusimamia vizuri utekelezaji.

"Nimpongeze Mhe. Rais kwa kutoa fedha kwa mradi huu kwani maji hayana mmbadala, Niipongeze Wizara ya Maji, mnafanya kazi nzuri sana katika miradi ya maji, tunaambiwa kwenye ripoti na tunaona kwa macho kazi inavyoendelea, tumeenda Ruangwa kule Lindi tumeona, tumeenda Singida tumeona, tumeenda Mpanda tumeenda kila mahali tumeona miradi mikubwa ya fedha nyingi inaendelea vizuri. Nikupongeze Mhe. Aweso, na Katibu Mkuu mnafanya kazi nzuri sana, mmefuta visima hewa, mmefuta miradi hewa" Waziri Mkuu Dkt. Nchemba amesema.

Ametoa agizo kwa wakandarasi wote nchini wanaotekeleza miradi ya maji kuhakikisha



ikiwemo vibarua kwakuwa serikali imeshatekeleza jukumu lake la kutoa fedha kwa Mkandarasi.

Ametoa angalizo kwa wakandarasi wote watakaoshindwa kutekeleza hawatopewa tena mradi hapa nchini.

Kwa upande wake, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema Wizara ya Maji itahakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati ili wananchi waweze kunufaika. “Kupitia Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka fedha nyingi na tayari vijiji 10,758 vimeshafikiwa na huduma ya maji safi na salama na vimebaki vijiji 1,575.”



Mradi huo unatekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Maji  utahudumia wananchi zaidi ya elfu 60 wa Msanga, Buigiri, Mtumba na Chamwino.

 Utekelezaji wa mradi umefika asilimia 70.2 na utazalisha lita za maji milion 7.7 kwa siku na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 91 hadi asilimia 100.

Mahitaji ya maji katika eneo hilo  ni lita milioni 7.5 kwa siku wakati upatikani wa sasa wa maji kwa siku ni lita milioni 4.8





# AWESO ASISITIZA UWAJIBIKAJI NA WELEDI KUWA AGENDA KUU KWA WIZARA YA MAJI

**Mtumba**, Dodoma

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amewataka watumishi wa Sekta ya Maji nchini kuongeza bidii, weledi na uwajibikaji ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Amesisitiza kuwa upatikanaji wa maji safi na salama ni nguzo muhimu ya maendeleo ya jamii na uchumi kukua hivyo kila mtumishi anapaswa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kujituma

Akizungumza na Menejimenti ya Wizara ya Maji na RUWASA katika ukumbi wa Wizara ya Maji Mtumba, jijini Dodoma, Mhe. Aweso amebainisha kuwa mafanikio yanategemea mshikamano na ushirikiano wa dhati miongoni mwa watumishi.

Amesisitiza kuwa viongozi wanapaswa kuwa mfano bora kwa kuzingatia maadili ya kazi, uwazi na uwajibikaji, sambamba na kuimarisha mawasiliano katika taasisi.

Waziri Aweso amepongeza menejimenti kwa kazi nzuri na ushirikiano katika suala la ukaguzi wa kazi za Sekta ya Maji na kueleza , ni mafanikio hayo yanaonyesha matumizi sahihi ya rasilimali za umma pamoja na usimamizi imara wa miradi ya maendeleo. Amewataka watumishi kuendeleza viwango hivyo na kujipambanua zaidi katika utendaji wao.





Amehimiza matumizi ya ubunifu pamoja na utekelezaji wa mkakati madhubuti wa kukabiliana na changamoto zilizopo, kukamilisha miradi kwa wakati na kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wote. Amesema kuwa Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuongeza ufanisi katika sekta.

Katika hatua nyingine, ameipongeza RUWASA kwa juhudi kubwa za kushughulikia changamoto za wananchi kwa wakati, hatua inayochangia kuimarisha imani ya wananchi na kuboresha huduma ya maji vijijini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, amewataka watumishi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kushirikiana kwa karibu na kuweka mbele maslahi ya wananchi ili kuhakikisha huduma ya maji inaboreshwa na kuwa endelevu kwa manufaa ya sasa na kizazi kijacho.





# BENKI YA DUNIA YAIPONGEZA SERIKALI HUDUMA YA MAJI

**Dodoma**, Tanzania

**Benki ya Dunia (WB) imeipongeza Serikali katika huduma ya maji kwa wananchi.**

Pongezi hizo zimeelekezwa Wizara ya Maji katika kikao jijini Dodoma. Ni pongezi mahususi kwa kuwa kinara wa kuigwa barani Afrika katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini kupitia mfumo wa malipo kwa matokeo (P4R) katika kikao kilichowakutanisha Menejimenti ya Wizara ya Maji na ujumbe kutoka WB.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi wa Kanda wa Benki ya Dunia Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bi. Anna Wellenstein amesema Tanzania imefanikiwa kutekeleza kwa ufanisi miradi mbalimbali ya maji vijijini inayofadhiliwa na WB kupitia mfumo wa P4R, hatua ambayo imeonesha mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mtandao wa Taifa wa Usambazaji Maji.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri ya ushirikiano kati ya Serikali na wadau wa maendeleo, hali inayowezesha utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

Waziri Aweso ameielekeza Menejimenti ya Wizara ya Maji kuendelea kuimarisha ushirikiano na WB ili kuhakikisha miradi yote ya maji inakamilika kwa wakati na kuendelea kusogeza mbele azma ya Serikali ya kuhakikisha vijiji vyote nchini vinapata huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2030.





Kikao hicho pia kilijadili mafanikio ya ushirikiano kati ya Wizara ya Maji na WB pamoja na vipaumbele vya hatua inayofuata katika maendeleo ya Sekta ya Maji kuelekea utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Ujumbe wa Benki ya Dunia uliambatana na Bi. Soma Ghosh Moulik, Meneja wa Sekta ya Maji, Bi. Zhimin Mao, Mtaalamu wa Rasilimali za Maji, Bw. Ernest Ruzindaza, Mchumi Mkuu pamoja na Luth Kennedy-Walker, Mratibu wa Miradi ya Benki ya Dunia.






# SEKTA YA MAJI NA MAFANIKIO KATIKA MIRADI

Wizara ya Maji imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Mhandisi Mathew Kundo (Mb), amewapongeza watumishi wa Sekta ya Maji kwa mchango wao katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Amesema mafanikio yamechochewa na juhudi za watumishi pamoja na uwekezaji mkubwa wa Serikali.

Ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la Wizara ya Maji na taasisi zake katika maonesho ya kuelekea Siku ya Mazingira Duniani katika Viwanja vya Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Jijini Dodoma.



Ametaja miongoni mwa mafanikio hayo ni utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Kidunda wenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 330 pamoja na miradi mingine inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi.

Mhandisi Kundo amemshukuru Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha utekelezaji wa zaidi ya miradi 1,206 ya maji yenye thamani ya takriban Shilingi trilioni nne, inayolenga kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama nchini na kufanikisha azma ya kuwafikishia wananchi huduma hiyo.

Amewataka watalaam wa Sekta ya Maji kuendelea kutafuta vyanzo vipya vya maji na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza, kuendeleza na kuhifadhi vyanzo vya maji vilivyopo ili kuhakikisha huduma hiyo inakuwa endelevu.




Maonesho hayo yanatarajiwa kuhitimishwa kesho, Juni 5, 2026, ambapo Makamu wa Rais, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.



# WABUNGE WAONYESHWA MWELEKEO WA MKAKATI GRIDI YA MAJI YA TAIFA NA MANUFAA KWA WANANCHI

**Bungeni,** Dodoma



Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameshiriki katika semina kuhusu Mpango Mkakati wa Gridi ya Maji ya Taifa.

Semina hiyo imefanyika katika ukumbi wa Bunge wa Msekwa,Dodoma.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri katika mada yake amesema Gridi ya Maji ya Taifa ni mfumo wa kimkakati wa usambazaji maji kutoka kwenye vyanzo vya uhakika na kuyapeleka katika maeneo yenye uhaba wa maji nchini.

Ameongeza kuwa hadi sasa Wizara ya Maji imekamilisha vipande vya mtandao wa Taifa wa maji ikiwamo kutoa maji ziwa Victoria kwenda mikoa ya Shinyanga, Tabora na Shelui katika mkoa wa Singida.





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akihitimisha mada amewaomba ushirikishwaji wa jamii na ushirikiano kwa wabunge wote ili kuhakikisha mpango mkakati wa Gridi ya Maji ya Taifa unafanikiwa ili kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma ya majisafi na salama na kuchochea ukuaji wa uchumi ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (DIRA 2050).





# MHANDISI MWAJUMA WAZIRI ATUNUKIWA TUZO YA UTUMISHI WA UMMA ‘MALKIA WA NGUVU

**Dodoma**, Tanzania

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, ametunukiwa Tuzo ya Utumishi wa Umma katika kilele cha utoaji wa Tuzo za Malkia wa Nguvu kwa Kanda ya Kati, zilizofanyika jijini Dodoma.

Tuzo hiyo imetolewa na Kampuni ya Habari na Burudani ya Clouds tarehe 26, Aprili 2026, ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wa wanawake walioonesha utendaji uliotukuka katika sekta mbalimbali nchini.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, alikuwa mgeni rasmi katika sherehe hizo zilizowakutanisha wadau wa maendeleo, viongozi wa serikali na wanawake wajasiriamali.

Akizungumza katika hafla hiyo, Makamu wa Rais Dkt. Nchimbi amewapongeza washindi wote na kuishukuru Clouds Media Group kwa kuendelea kuibua na kutambua juhudi za wanawake nchini.

Aidha, amewataka Watanzania kuachana na dhana potofu ya kumchukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu, badala yake watambue mchango mkubwa wa wanawake katika kukuza uchumi wa Taifa.



Akimtaja Mhandisi Mwajuma Waziri kama mfano, amesema ni kielelezo cha mwanamke shupavu aliyebadilisha utendaji kazi na kuleta matokeo chanya katika sekta ya maji.



Amesisitiza kuwa Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake kushika nafasi za uongozi na kufanya vizuri katika utumishi wa umma.

Tuzo za Malkia wa Nguvu kwa mwaka huu zimejikita katika kuwatambua wanawake walioleta mabadiliko makubwa katika jamii kupitia nyanja za uongozi, biashara na huduma za kijamii.







# WADAU WA MAENDELEO KUSHIRIKISHWA UIMARISHAJI HUDUMA YA MAJI MWANZA

**Mwanza**, Tanzania

Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi jijini Mwanza.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amefanya kikao na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini Tanzania, Mhe. Christine Grau, kujadili hatua za utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maji na Usafi wa Ziwa Victoria (LVWATSAN).

Amesema Serikali inathamini mchango mkubwa wa EU katika sekta ya maji, na Jijini Mwanza ambako mahitaji yanaongezeka kutokana idadi ya watu na ukuaji wa mji.

Ametoa shukrani kwa EU kwa ushirikiano utakaowezesha MWAUWASA kumaliza changamoto ya mgao wa maji na kupanua wigo wa huduma.

Balozi wa EU nchini Mhe. Grau amesema umoja huo umeridhishwa na hatua zinazochukuliwa katika kuboresha utoaji huduma na kuimarisha uwazi, na wapo tayari kuunga mkono juhudi hizo.



EU na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (AFD), kwa kushirikiana na Wizara ya Maji wanatarajia kusaini Hati ya Makubaliano yenye thamani ya takribani Euro milioni 12.5.

Makubaliano hayo yatawezesha upatikanaji wa fedha kuanza utekelezaji wa programu ya LVWATSAN Awamu ya Pili, ikijumuisha upanuzi wa mtandao wa mabomba, ujenzi wa miundombinu na uboreshaji wa mfumo wa majitaka Jijini Mwanza.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda, ameeleza kuwa usafi wa mazingira ni eneo muhimu la uwekezaji, hususan kwa wakazi wanaoishi maeneo ya miinuko na pembezoni mwa jiji.

EU ni mdau wa maendeleo anayeshirikiana na Wizara ya Maji katika utekelezaji wa miradi ya majisafi na usafi wa mazingira.





# BILIONI 60.7 KUBORESHA HUDUMA ZA MAJI TUNDUMA NA VWAWA-MLOWO

**Dodoma,** Tanzania

Serikali ya Tanzania imesaini mkataba wa ruzuku na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani wa thamani ya shilingi bilioni 60.7 kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tunduma na Vwawa - Mlowo.

Hafla hiyo imefanyika katika ukumbi wa Wizara ya Fedha, jijini Dodoma

Mkataba huo utawezesha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata jumla ya Euro milioni 20, sawa na shilingi za Bilioni 60.7, kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW).

Hafla hiyo imehudhuriwa n Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, ambaye ameishukuru Serikali ya Shirikisho la Ujerumani kwa kuendelea kuiunga mkono Tanzania katika maendeleo ya Sekta ya Maji kupitia ruzuku hiyo muhimu.

Amesema utekelezaji wa mradi huo utaimarisha usimamizi wa rasilimali za maji unaozingatia athari za mabadiliko ya tabianchi na kuboresha upatikanaji wa huduma za majisafi, salama na za uhakika kwa wananchi wa maeneo husika.

“Mradi huu unaendana kikamilifu na vipaumbele vya maendeleo vya Serikali, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Sera ya Taifa ya Maji, pamoja na dhamira ya Tanzania ya kufikia Lengo la Sita la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 6) kuhusu upatikanaji wa maji safi na huduma bora za usafi wa mazingira,” Mhandisi Waziri amesema.

Mradi huo unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira, kuboresha afya za wananchi pamoja na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika miji ya Tunduma na Vwawa-Mlowo.



# MITI YAOTESHWA BUTIMBA SIKU YA ZIWA VICTORIA

**Mwanza**, Tanzania

Wananchi katika mkoa wa Mwanza wameshiriki kampeni ya kutunza vyanzo vya maji katika ziwa Victoria kwa kuanza kuotesha miti elfu mbili katika chanzo cha maji cha Butimba.

Mkuu wa mkoa wa Mwanza Said Mtanda ameongoza zoezi hilo ambapo miti rafiki wa maji imeoteshwa kuashiria uzinduzi wa kampeni ya kuotesha miti kuelekea siku ya ziwa Victoria ambayo inaadhimishwa kwa mara ya kwanza Jijini Mwanza.



Amesema ziwa Victoria linanufaisha watu zaidi ya milioni 45 wa Afrika Mashariki hivyo ni muhimu kuhakikisha linahifadhiwa na kuendelezwa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Amesema kupanda miti ni kumbukumbu kubwa inayodumu hata aliyepanda anapokuwa hayupo.

Amewataka wananchi wote kuhakikisha wanaendelea kuotesha miti katika vyanzo vyote vya maji, makazi na maeneo mbalimbali kwasababu miti ni mazingira, mazingira salama ni maisha salama.

Zoezi la kuotesha miti limewashirikisha viongozi mbalimbali akiwamo Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Rose Ambrose ambaye amesisitiza umuhimu wa kuotesha miti katika vyanzo vya maji vyote nchini. Amesema Wizara ya Maji kupitia Bonde la Ziwa Victoria inakusudia kuotesha miti 10,000. Ambapo miti 6500 imeshaoteshwa. Aidha pamoja na miti 2000 iliyooteshwa, Wizara ya Maji inakusudia kuotesha miti 5000 katika maadhimisho ya siku ya Ziwa Victoria ambayo ni Mei 21.



Amesema chanzo cha maji cha Butimba ni muhimu kwa maisha ya wakazi wa Mwanza kwasababu chanzo hicho kinazalisha lita za maji kwa siku milioni 48 na kunufaisha zaidi ya wananchi 450,000. Lengo ni kukiendeleza ili kifikie uzalishaji wa maji lita milioni 96 ambazo zitakuwa zikinufaisha wakazi laki nane.

Naye Katibu Mtendaji Kamisheni ya Bonde la ziwa Victoria Dkt. Masinde Bwire amesema zoezi la kuotesha miti katika kutunza ziwa Victoria linafanyika kwa nchi zinazounda kamisheni hiyo zikiwemo Kenya, Uganda Burundi na Rwanda

Amesisitiza ushirikiano kwa kila mmoja ili kuhakikisha ziwa hilo linadumu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.





# KATIBU MKUU MAJI AITAKA DAWASA KUFUNGA MKANDA MAPAMBANO UPOTEVU WA MAJI

**Dar es salaam**, Tanzania

Baraza kuu  la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) limekutana kujadili na kuweka mwelekeo wa vipaumbele vya DAWASA kuelekea mwaka wa fedha 2026/2027, likilenga kuimarisha utoaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi.

Akizungumza katik kikao kazi hicho, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, amesema Baraza la wafanyakazi ni jukwaa muhimu la mawasiliano linalowaunganisha Menejimenti na watumishi katika kupanga mikakati ya kuboresha huduma kwa wananchi.



“Niwashukuru kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika tukio hili. Ni matumaini yangu kuwa majadiliano yenu yatajikita katika kukabiliana na changamoto ya upotevu wa maji ili kuimarisha huduma na kuokoa mapato yanayopotea,” Mhandisi Mwajuma amesema..

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa DAWASA, Mhandisi Romanus Mwangingo, amesema kipaumbele kikuu cha DAWASA kwa sasa ni kukabiliana na changamoto ya upotevu wa maji (NRW), akibainisha kuwa tayari hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa.

“Tunawekeza katika kupunguza upotevu wa maji kwa kununua mita za malipo ya kabla kwa ajili ya wateja na kubadilisha miundombinu chakavu ambayo imekuwa ikichangia upotevu huo,” amesema Mhandisi Mwangingo.

Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire, amewashukuru viongozi wa Sekta ya Maji kwa kushiriki katika uzinduzi wa kikao hicho, na kuwataka wajumbe wa Baraza la wafanyakazi kushirikiana kikamilifu katika utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa.

***"Ni muhimu kila mmoja wetu akawa sehemu ya suluhisho kwa kutoa elimu kwa watumishi wenzake ili kusimama kwa pamoja katika kukabiliana na changamoto ya upotevu wa maji,"*** amesema Mhandisi Bwire.





# MORUWASA YASAINI MKATABA WA MFUMO WA KIDIGITALI WA KUDHIBITI UPOTEVU WA MAJI MANISPAA YA MOROGORO

**Morogoro,** Tanzania

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imesaini mkataba wa utekelezaji wa mradi wa kisasa wa kidigital wa kuthibiti upotevu wa maji, Smart Non-Revenue Water (NRW) Management System kwa kushirikiana na asasi ya World Waternet, ikiwa ni hatua madhubuti ya kupambana na upotevu wa maji na kuboresha huduma kwa wananchi.

Akizungumza mara baada ya utiaji saini wa mkataba huo, Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, CPA Sais Kyejo, ameishukuru World Waternet kwa ushirikiano huo na kusisitiza kuwa Mamlaka itaulinda ili kuhakikisha unaleta manufaa chanya kwa wakazi wa Morogoro.

Mradi huo utatekelezwa katika eneo la Mazimbu pamoja na kituo cha kusukuma maji cha Tumbaku, ukihusisha matumizi ya teknolojia za kisasa kama Akili Unde (AI) na mtandao wa mawasiliano, Internet of Things (IoT) kwa ajili ya ufuatiliaji wa mtiririko wa maji kwa wakati halisi, kubaini uvujaji, kubaini maeneo yanayokabiliwa na upotevu wa maji na kuongeza ufanisi wa mfumo wa usambazaji.

Kupitia utekelezaji wa mradi huo, MORUWASA inatarajia kupata takwimu sahihi za matumizi ya maji, kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza upatikanaji wa huduma endelevu, hatua itakayochochea maboresho ya huduma za maji katika Manispaa ya Morogoro.






# UCHIMBAJI HOLELA WA VISIMA NI HATARI KWA USALAMA WA MAJI ARDHINI.

**Dar s salaam,** Tanzania

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kutumia rasilimali za maji kwa uangalifu, ili kuhakikisha maji yanaendelea kupatikana kwa sasa na kwa vizazi vijavyo.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, Mhandisi Elibariki Mmassy, katika mahojiano aliyofanya katika radio ya Crown amesisitiza kuwa wananchi wanapaswa kufuata taratibu za kisheria ikiwa ni pamoja na kuombaji wa vibali vya matumizi ya maji na uchimbaji wa visima.

Ameongezea kuwa kupata kibali husaidia kuhakikisha uchimbaji wa visima unafanyika kwa kufuata taratibu za kitaalamu na kisheria, hivyo kuepusha uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na kupunguza hatari ya uchafuzi na ubora wa maji chini ya ardhi.

Katika hatua nyingine, Mhandisi Mmassy ameongeza kuwa Mto Ruvu ni chanzo kikuu cha maji kinachochangia upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya jirani, hivyo wananchi wanapaswa kuepuka vitendo vitakavyoharibu chanzo hicho kama vile kutupa taka ovyo, kukata miti holela na kufanya shughuli za kibinadamu au kibiashara karibu na mto.

Ametumia wasaa huo kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji kwa kuanza ujenzi wa Mradi wa bwawa la Kidunda, ambao utakapokamilika unatarajiwa kumaliza changamoto za upatikanaji wa huduma za maji safi na salama katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

***"Tone la maji lazima lihifadhiwe."***





# MKANDARASI ATAKIWA KUONGEZA KASI MRADI WA MAJI MIJI 28 MAFINGA

**Njombe,** Tanzania

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Rose Ambrose, amemtaka mkandarasi wa Mradi wa Maji wa Miji 28 Mafinga kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo ili wananchi wa Mafinga na maeneo jirani waanze kupata huduma ya majisafi na salama.

Bi. Rose amesema hajaridhishwa na maendeleo ya mradi huo na kusisitiza kuwa hakuna sababu ya kuchelewesha utekelezaji wake. Amesema Serikali inahitaji kuona kazi muhimu ikiwemo ujenzi wa bwawa na miundombinu mingine ikiendelea kwa kasi.

Aidha, amemtaka mkandarasi huyo kuwasilisha Wizara ya Maji mpango kazi wa haraka utakaobainisha namna atakavyoongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo hadi kukamilika kwake kwa wakati.

Ameeleza kuwa Serikali haitakubali kuona mradi huo ukiendelea kusuasua kwani unalenga kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa Mji wa Mafinga na maeneo ya jirani.

Mradi huo unatarajiwa kunufaisha zaidi ya wananchi 109,720 wa kata saba za Halmashauri ya Mji wa Mafinga na kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama kutoka asilimia 67 hadi 89.



# TANZANIA NA KOREA KATIKA MPANGO WA USIMAMIZI WA KISASA WA MAJITAKA

**Dodoma,** Tanzania




Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, amefungua kikao cha wataalamu wa Wizara hiyo pamoja na ujumbe kutoka Jamhuri ya Korea, ukiongozwa na wataalamu kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA), kwa lengo la kujadili maandalizi ya Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Majitaka kwa kutumia mifumo ya kisasa, rafiki kwa mazingira na inayozingatia mabadiliko ya tabianchi.

Wakati wa ufunguzi wa kikao hicho jijini Dodoma, Mhandisi Mwajuma amewataka wataalamu wa Wizara ya Maji kutumia fursa hiyo kujadiliana kwa kina na wenzao kutoka Korea ili kubaini manufaa ya mradi huo kwa wananchi, pamoja na kuhakikisha kuwa utekelezaji wake unalinda mazingira na kuchangia kufanikisha maono ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

"Tumeendesha majadiliano kwa takribani wiki mbili na wataalamu hawa kutoka Korea. Ni matarajio yangu kuwa kikao hiki kitazaa matokeo yenye tija kwa nchi yetu. Tunaamini kuwa kupitia ushirikiano huu, tutapata mafanikio katika kuboresha usimamizi wa majitaka na hivyo kuleta manufaa kwa wananchi," amesema Mhandisi Mwajuma.

Katika kikao hicho, wataalamu wamejadili kwa kina matumizi ya mifumo ya Climate Smart-DEWATS (Decentralized Wastewater Treatment Systems), ambayo inalenga kuboresha usimamizi wa majitaka katika ngazi ya jamii kwa ufanisi na uendelevu. Mifumo hii ina sifa ya gharama nafuu katika ujenzi na uendeshaji, matumizi madogo ya nishati, pamoja na urahisi wa uendeshaji na matengenezo.

Aidha, mifumo hiyo inawezesha uzalishaji wa nishati mbadala kupitia biogas, urejelezaji wa mabaki ya majitaka (sludge) kuwa mbolea, pamoja na matumizi ya maji yaliyotibiwa kwa shughuli za kilimo. Hali hii inaimarisha dhana ya uchumi mzunguko (circular economy) kwa kutumia rasilimali kwa ufanisi zaidi na kupunguza athari kwa mazingira.

Pamoja na majadiliano hayo, wataalamu kutoka KOICA wameendelea kuwajengea uwezo wataalamu wa Wizara ya Maji kwa kuwapatia uzoefu na ujuzi kuhusu utekelezaji wa miradi ya usimamizi wa majitaka iliyofanikiwa katika nchi mbalimbali.

Mradi huo unaofanyiwa maandalizi unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mji wa Karatu kama eneo la mfano (pilot project), kabla ya kupanuliwa katika maeneo mengine.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa KOICA nchini Tanzania, Bw. Sikhyin Kim, amesema kuwa ushirikiano kati ya Jamhuri ya Korea na Tanzania katika sekta mbalimbali za maendeleo, ikiwemo huduma ya maji, ni wa muda mrefu na umeendelea kuleta matokeo chanya kwa wananchi.

Ameongeza kuwa ushirikiano huo utaendelea kuimarishwa ili kuhakikisha maendeleo endelevu yanapatikana kwa manufaa ya pande zote mbili.



# MRADI WA MAJISAFI, NALA WAZINDULIWA NA MBIO ZA MWENGE - DODOMA

**Dodoma,** Tanzania

Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2026, zimezindua Mradi wa Majisafi wa Nala Jijini Dodoma unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA).

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Ndugu Wazo Mwang'onda akiongea na wananchi amesema mradi huo umekidhi vigezo vya utekelezaji wake.

Amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo wa majisafi ambao umemtua mama ndoo kichwani.

Mradi wa Majisafi Nala tayari unahudumia wakazi zaidi ya 5,188 katika maeneo ya Nala Center, Segu Juu, Chihoni na Kiwanda cha Mbolea cha Nala cha Itracom.





# WADAU WA SEKTA YA MAJI WAJADILI MAENDELEO YA SEKTA

**Mtumba,** Dodoma



Wadau wa Sekta ya Maji nchini wamakutana kujadiliana maendeleo ya Sekta ya Maji.

***Kikao kimefanyika katika Ofisi za Wizara ya Maji, Mtumba Jijini Dodoma.***

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara Ya Maji Bi. Rose Zacharia Ambrose akifungua kikao amesema Sekta ya Maji ndiyo nguzo muhimu katika kuhakikisha mipango iliyopangwa inakuwa endelevu na kutimia.

Amesema ni muhimu kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji na maendeleo yaliyofikiwa.

Bi. Rose amesema Wizara ya Maji inatambua uwepo wa changamoto ya kifedha katika kutekeleza miradi mbalimbali, ikiwemo ya utafiti wa vyanzo vya maji nchini na inatumia vyanzo mmbadala kufanikisha hilo.

Amewataka wadau wa Sekta ya Maji nchini kuandaa mkakati kufanikisha miradi ya maji.

Katika kikao hicho imeelezwa kuwa mojawapo ya changamoto zinazoikabili Sekta ya Maji ni pamoja na ongezeko la mahitaji ya huduma ya maji, mabadiliko ya tabianchi.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Rasilimali za Maji, Bw. Robert Sunday amesema lengo la serikali ni kuhakikisha huduma ya ni yenye ubora kwa matumizi, na maji kuwa chanzo kikubwa cha kuchochea ukuaji wa uchumi nchini.

Pamoja na mambo mengine kikao hicho kimejadili changamoto, mafanikio ya Sekta ya Maji na mpango mkakati ya kutekeleza malengo ya sekta kwa miaka ijayo Ili kuboresha huduma za maji nchini.







# GWANDI WAPATA MAJI

Serikali imewezesha huduma ya maji ya uhakika kwa wakazi wa kijiji cha Gwandi, Wilaya ya Chamwino mkoa wa Dodoma.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Mhe. Eliasi Kawweya, amesema mradi huo ni miongoni mwa miradi 18 inayotekelezwa na asasi ya Water Mission mkoani Dodoma ambapo ni faraja kwa wakazi wa Gwandi.

Mhe. Kawweya amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweka mazingira wezeshi yanayowashirikisha wadau wa maendeleo katika kazi za maendeleo.

Meneja wa mkoa wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Mbarak Ally Rajabu, amepongeza wadau wa maendeleo kwa kufanikisha mradi huo.

Amesema hadi sasa, kijiji kimoja katika wilaya hiyo hakijafikiwa na huduma ya maji safi na salama, ila kimejumuishwa katika mpango wa bajeti ya 2026/27.

Amesema kuwa mradi umewekewa Dira za malipo kabla (pre-paid water meters) katika vituo vyote vya umma vya kuchotea maji pamoja na birika la kunyweshea mifugo. Mfumo huo utasaidia kudhibiti matumizi ya maji na kuondoa malalamiko ya ankara.

Amewaasa wananchi kutunza Dira hizo na kuhakikisha wanalipia huduma kadri wanavyotumia kuepuka usumbufu wa kukatika kwa maji.

Mradi umegharimu kiasi cha shilingi milioni 577.5, ambapo shilingi milioni 561 zimetolewa na asasi ya Water Mission, na shilingi milioni 16.5 kutoka kwa wananchi.

Mradi huo una mtandao wa mabomba wenye urefu wa kilomita 21.3, na unatarajia kuwanufaisha zaidi ya elfu tano katika kijiji cha Gwandi kwa sasa, hadi kufikia zaidi ya wananchi elfu 7.6 kwa miaka ijayo.





# MAJI WAKESHA MWANZA KUPATA SULUHU YA HUDUMA

**Mwanza,** Tanzania

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amefika mkoani Mwanza mapema na kuanza kazi ya kuimarisha huduma ya maji kwa wakazi wa jiji la Mwanza.



Amefika katika kituo cha kusukuma maji cha Capripoint na kuongoza kikao na Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), kabla ya kukagua hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi.

Kikao hicho dhamira yake ikiwa kupata picha halisi ya hali ya huduma ya majisafi, kubaini changamoto zilizopo, na kuandaa mpango wa hatua za haraka na za kudumu za kuboresha huduma.

Waziri Aweso amewataka wataalamu wa Wizara ya Maji na MWAUWASA kukesha wakifuatilia na kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji unaimarika.

Aliahidi kutembelea maeneo kadhaa kujionea hali halisi, ikiwemo chanzo kikuu cha maji cha Butimba .



# KATIBU WAKUU WAKUTANA KUHUSU UTEKELEZAJI WA AGIZO LA WAZIRI MKUU

**Dodoma,** Tanzania

Katibu Wakuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara za Fedha, Afya na Maji, wamekutana jijini Dodoma mahsusi kuhusu utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba kuhakikisha huduma ya majisafi na salama inafika katika shule na vituo vya afya nchini.

Hatua hiyo inafanyika ikiwa ni maandalizi ya Mpango wa Kuboresha Huduma za Maji, Usafi wa Mazingira na Usafi wa Mtu Binafsi (Presidential WASH Compact).

Mpango unalenga kuhakikisha huduma za majisafi, usafi wa mazingira na usafi wa mtu binafsi zinapatikana kwa uhakika, usawa na ubora nchini ifikapo 2030.

WASH Compact ni mkataba unaobeba ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, unaolenga kuimarisha usalama wa maji na utoaji endelevu wa huduma za maji, usafi wa mazingira na usafi wa mtu binafsi.

Mkataba huo unaainisha matokeo yanayotarajiwa, mageuzi ya kisekta, uwekezaji unaohitajika pamoja na misingi ya uwajibikaji.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri akiongoza kikao amesema lengo kuu la kikao hicho ni kujenga uelewa wa pamoja miongoni mwa sekta mtambuka zinazotekeleza WASH kabla ya kuanza rasmi kwa utekelezaji.





“Ni muhimu kwa sekta zote kushirikiana na kuwa na uelewa wa pamoja ili kuhakikisha mpango huu unatekelezwa kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya,” Mhandisi Mwajuma amesema.

Ameongeza, licha ya Sekta ya Maji kuwa mhimili muhimu wa maendeleo, mafanikio ya mpango huo yanategemea ushirikiano madhubuti kati ya sekta zote husika.

Kikao kimewahusisha wataalamu kutoka wizara mbalimbali pamoja na wataalamu washauri wa mpango huo, ambao wamesisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano wa kisekta ili kufanikisha utekelezaji wake.

Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya huduma ya maji, hususan maeneo ya vijijini na yenye uhitaji mkubwa, pamoja na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidigitali katika utoaji wa huduma.

Viongozi hao wamejadili mbinu za kuhakikisha upatikanaji endelevu wa rasilimali fedha, ikiwemo ushirikishwaji wa sekta binafsi na washirika wa maendeleo katika utekelezaji wa mpango huo.

Mpango katika utekelezaji utajikita katika nguzo kuu tatu ; kuongeza upatikanaji wa huduma za WASH katika maeneo mbalimbali kama kaya, shule na vituo vya afya, kuimarisha mifumo ya utoaji huduma pamoja na kuboresha mbinu za upatikanaji wa rasilimali fedha.

Mpango wa WASH Compact ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuharakisha maendeleo ya jamii na uchumi, ukitarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika ustawi wa maisha ya wananchi.



# UJENZI WA MTAMBO WA KISASA WA KUCHAKATA MAJI TAKA WA MBEZI BEACH JIJINI DAR ES SALAAM

Utekelezaji wake umefika asilimia 70 ambapo mradi ukikamilika katika awamu ya kwanza utakuwa na uwezo wa kuchakata maji taka yenye ujazo wa mita za ujazo 16,000 kwa siku kwa kuhudumia maeneo ya Mbezi Beach na Kawe.

Mradi utaongezewa  uwezo wa kuchakata maji taka hadi kufikia mita za ujazo elfu 22 kwa siku ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya huduma za usafi wa mazingira katika maeneo hayo.





# WABUNGE WAKITOA MCHANGO NA MAONI KUHUSU HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA MAJI 2026/27 BUNGENI JIJINI DODOMA.

Wabunge wakitoa mchango na maoni kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji 2026/27 Bungeni jijini Dodoma.

Hoja, maoni na michango imelenga kuboresha mpango wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele hususan upatikanaji wa majisafi na salama, utekelezaji wa miradi ya maji vijijini na mijini, pamoja na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji nchini.







# BWAWA LA FARKWA MBIONI UJENZI

**Chemba**,Dodoma

Serikali inaendelea na hatua za awali za ujenzi wa bwawa la Farkwa ambapo Wizara ya Maji kupitia programu ya Uhimilivu dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi na Uboreshaji wa huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DSRSWSP) inahamisha nyenzo katika maeneo ya umma ikiwemo shule.

Zoezi linafanyika kwa kushirikiana na ofisi za mamlaka za Serikali za Mitaa wilaya ya Chemba, mkoa wa Dodoma.



Nyenzo zinazohamishwa zinatoka shule ya msingi Bubutole na shule ya msingi Mombose na kupelekwa katika shule mpya ya Sankwaleto kuboresha miundombinu.

Kinachoendelea kwa sasa ni kukusanya na kusafirisha.

Zoezi hilo ni endelevu kwa Wizara ya Maji kupitia program ya DSRSWSP na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kuandaa eneo la mradi.

Mradi wa bwawa la Farkwa unafadhiliwa na AfDB.



# WIZARA YA MAJI WAKAGUA CHANZO CHA MAJI CHA MAKUTUPORA

**Makutupora,** Dodoma



Wizara ya Maji imekagua chanzo cha maji cha Makutupora ambacho kinategemewa katika jiji la Dodoma

Ukaguzi umeongozwa na watalaamu wa Idara ya Rasilimali za Maji kwa kushirikiana na Bodi ya Maji Bonde la Wami-Ruvu pamoja na Bodi ya Maji Bonde la Kati, ikiwa ni sehemu ya kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

Lengo mahsusi limekuwa kuongeza ufanisi katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maji, na kutumia kama jukwaa la mafunzo kwa watumishi.

Ukaguzi umewezesha, watumishi kupata fursa ya kujifunza kwa vitendo kuhusu usimamizi wa maji chini ya ardhi, mbinu za ufuatiliaji wa vyanzo vya maji pamoja na namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.

Chanzo cha maji cha Makutupora bado kinaendelea kuwa tegemeo kuu la upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Jiji la Dodoma,

Ni rasilimali nyeti inayohitaji uangalizi na usimamizi wa karibu zaidi. Kutokana na umuhimu huo, ziara hiyo imebainisha haja ya kuimarisha tathmini za rasilimali za maji, kuongeza matumizi ya tafiti za kisayansi pamoja na kuendeleza mifumo madhubuti ya kufuatilia hali ya maji chini ya ardhi.

“Dodoma ni Makutupora na Makutupora ni Dodoma”

"1 5 7 5: Maji, Tuko Site, Kikazi Zaidi"







# WAFANYAKAZI WAPATA VIONGOZI

**Mtumba,** Dodoma

Viongozi wa Chama Cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) Tawi la Wizara ya Maji wamechaguliwa.

Uchaguzi huo wa viongozi wapya wa Halmashauri ya Tawi kwa mwaka 2026- 2031 ni Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wa halmashari. Uchaguzi umefanyika katika ukumbi wa Wizara ya Maji, Mtumba jijini Dodoma.

Matokeo kwa walioibuka washindi ni Mhandisi Mwanauwani Mbukuzi kuwa Mwenyekiti wa Tawi la wafanyakazi Wizara ya Maji na Katibu ni Mtunza Kumbukumbu Mkuu Ndugu James Ng'atigwa.




Akizungumza baada ya uchaguzi Mhandisi Mwanauwani amewashukuru wanachama na kuwapongeza wajumbe wapya waliochaguliwa na ameahidi kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuleta mabadiliko chanya hasa katika eneo linalo husu maslahi ya watumishi

Msimamizi wa uchaguzi huo Mwenyekiti wa TUGHE mkoa Bw.Maulid Kipeneku amesema ni muhimu kwa viongozi wa Tawi kuongeza jitihada katika kuongeza wanachama wapya hasa vijana ili kuleta chachu ya mabadiliko na kujenga mahusiano bora kati ya watumishi.



# TUZO YA MALKIA WA NGUVU NI YA WIZARA YA MAJI

**Mtumba,** Dodoma



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri, akipokelewa na Watumishi wa Wizara ya Maji katika mji wa serikali Mtumba, Dodoma

Mapokezi hayo yamefanyika baada ya Mhandisi Mwajuma kuibuka na tuzo ya Malkia wa Nguvu katika Utumishi wa Umma. Tuzo hizo ziliandaliwa na kampuni ya Clouds.

Baada ya kuwasili, Mhandisi Mwajuma alitoa neno la shukrani kwa watumishi wote wa Wizara ya Maji

" Tuzo hii ni yetu sote, bila Utumishi wa Wizara ya Maji pengine nisingepata tuzo hii, na utendaji wa wenu katika Wizara ya Maji ndio umeleta tuzo hii kwahiyo ninawashukuru sana watumishi wote na niwatie moyo tuendelee kuchapa kazi" Mhandisi Mwajuma amesema





2026/2027

# HOTUBA YA BAJETI 2026/2027











**Jumanne ya tarehe 05 Mei, 2026, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (Mb), aliwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2026/2027. Ufuatao ni muhtasari wa Bajeti hiyo ambayo imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26; Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP); Changamoto na hatua zinazochukuliwa; Vipaumbele na mwelekeo wa sekta kwa mwaka 2026/27, Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2026/27; na maombi ya fedha kwa mwaka 2026 2026/27.**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Maji**

# HOTUBA YA BAJETI WIZARA YA MAJI 2026/2027

**Kusoma na Kupakua Hotuba ya Bajeti Wizara ya Maji 2026/2027**

**SCAN HAPA**



*Limeandaliwa na*
**Kitengo cha Mawasiliano**


**Government City, Maji Street**
P.o.box 456, Dodoma

**Hotline :- +255 26 2322602**

**Fax No : +255 26 2322603**

**Email : Ps@maji.go.tz**

**Website ; www.maji.go.tz**